

Ujifunzaji wa Kiswahili Miongoni mwa Wakinga

Arnold B. G. Msigwa
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

Ikisiri

Lengo la makala haya ni kueleza dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa lugha ya pili (kuanzia sasa Lg2) katika Jamii ya Wakinga. Usasanyuzi dosari ni eneo muhimu katika taaluma ya Isimu Tumizi na katika taaluma ya ujifunzaji wa Lg2. Umuhimu wake unatokana na ukweli kwamba, wajifunzaji wengi wanaojifunza Lg2 hufanya dosari mbalimbali katika hatua ya kujifunza lugha hiyo. Vilevile, ni mbinu pangilifu ya kuchanganua dosari za mjifunzaji lugha. Kitaaluma dosari si kitu kibaya bali ni kipengele muhimu katika mchakato wa ujifunzaji lugha. Dosari husaidia kutambua mchakato changamani wa maendeleo ya lugha Na namna pangilifu ya kubaini, kueleza na kufafanua dosari za mjifunzaji lugha. Pia, dosari zinaweza kusaidia kutoa uelewa wa mchakato wa kuamili Lg2. Makala haya kwa hiyo yanalenga kuchunguza kwa nini wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii Wakinga hushindwa kumudu vema lugha ya Kiswahili licha ya kuwa ni somo la lazima tangu shule za msingi hadi sekondari za juu. Makala yanahitimisha kwamba dosari hizi kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na athari za lugha yao ya kwanza na umbali wa kijiografia kutoka kitovuni mwa lugha ya Kiswahili.

Maneno Muhimu: Usasanyuzi Dosari, Dosari, Makosa Na Uamiliaji Lugha

Utangulizi

Usasanyuzi Dosari ni kipengele katika taaluma ya Isimu Tumizi na katika ujifunzaji na ufundishaji wa Lg2. Isimu Tumizi ni taaluma inayoshughulikia changamoto mbalimbali zinzohusiana na ufundishaji na uamiliaji wa Lg2. Pia, taaluma hii inajaribu kutafuta suluhu changamoto hizi ili kuwezesha ufundishaji na uamiliaji wa Lg2 kuwa na tija. Usasanyuzi Dosari ni mkabala unaeleza uhusiano kati ya dosari za mjifunzaji lugha na mikakati ya ufundishaji wa Lg2, mazingira ya kujifunzia na mtazamo wa mjifunzaji Lg2 dhidi ya lugha na utamaduni wa lugha anayojifunza. Kwa maana hii, dosari za wajifunzaji wa Lg2 zina uhusiano na mikakati itumikayo kufundishia, mazingira ya kujifunzia na mtazamo wa mjifunzaji lugha. Miongoni mwa tafiti zenye mwelekeo

waKiusasanyuzi Dosari zilizoleta ufahamu wa kina kuhusiana na ujifunzaji na uamiliaji wa lugha ni pamoja na: James, (1989, 1998), Keshavarz, (2003; 2006), Darus (2009). Norrish (1983) Ellis (1995) na Ziahisseiny (1999). Matokeo ya tafiti hizi kwa kipindi kirefu yametumika kuonesha huo uhusiano ruwaza ya maendeleo ya mjifunzaji Lg2 na mikakati itumikayo kufundishia. Kwa mujibu wa Corder, (1967; 1971 na 1974) anadai kwamba, wajifunzaji wa Lg2 wanajifunza lugha hiyo sawa na wanavyojifunzawa lugha ya kwanza (kuanzia sasa Lg1). Hitimisho hili lilitokana na ukweli kwamba, watoto wanapoamili¹ Lg1 hufanya dosari nyingi. Kutokana na dosari hizo wanazofanya watoto, watafiti hawa wakahitimisha kwamba, ujifunzaji wa Lg2 hufanyika sawasawa na ujifunzaji wa Lg1 kwa kuwa nao unahusisha dosari nyingi miongoni mwa wajifunzaji wa Lg2. Lengo la makala haya ilikuwa ni kuchanguza dosari za kimuundo zinazofanywa na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wilaya ya Makete mkoa wa Njombe. Mtafiti alinua kubainisha dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa Lg2 katika jamii hii, kisha kufafanua chanzo cha sababu hizo. Katika kutimiza malengo hayo, maswali mawili ya utafiti yaliulizwa na kupatiwa majawabu yake: (i) Je, ni msamiati upi gani unaokuwa na dosari miongoni mwa wajifunzaji wa Lg2 katika jamii ya Wakinga? (ii) Ni sababu zipi zinasababisha kutokea kwa dosari hizo kwa wajifunzaji wa Lg2 katika jamii ya Wakinga?

Data zilikusanywa kwa njia ya kujaza hojaji na uandishi wa insha. Kazi ya mtafiti ilikuwa ni kuzipitia hojaji na insha hizo moja baada ya nyingine kisha kufanya tathmini kuhusu usahihi wake kimuundo na kimofolojia kwa kuzingatia kanuni za lugha ya Kiswahili. Ile miundo ya Lg2 iliyobainika kukiuka utaratibu wa Kiswahili sanifu ilichukuliwa kwamba mjifunzaji amefanya dosari. Utafiti huu ulikuwa ni wa kitaamuli kwa kiasi kikubwa na kwa kiasi kidogo tu ulikuwa wa kiidadi, hivyo mbinu za uchanganuzi maudhui zilitumika. Mbinu hii hutumika kuchanganua maudhui ya matini yoyote kwa kuangalia maudhui ya kila neno na maana zake. Aidha, usahihi wa maneno na maudhui yaliyotumika kuunda tungo vilizingatiwa kwa mujibu wa Kiswahili sanifu. Hivyo, kila matini iliyotumiwa na mjifunzaji Lg2 ilichunguzwa umbo lake na maana yake kwa kuzingatia kanuni za Kiswahili sanifu. Kujumla, mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu, ndiyo zile mbinu zinazotumika katika utafiti wa sayansi za jamii.

¹ Dhana hii ilipendekezwa na Krashan miaka ya 1970 ikiwa na maana ya mchakato wa kiisimu unaotokea kwa wajifunzaji wa lugha ya pili au ya Kigeni katika hali ya ung'amuzibwete, kwa maana hii kwamba, mjifunzaji lugha hung'amua kanuni za lugha pasipo kukusudia wala mwenyewe kufahamu kwamba jambo hilo linatokea.

Msingi wa Kinadharia

Ukusanyaji na uchanganuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Usasanyuzi Dosari Corder (1971). Wazo kuu la Nadharia ya Usasanyuzi Dosari ni kuwa, dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa Lg2 husababishwa na vyanzo mbalimbali ikiwamo athari za Lg1 katika Lg2. Katika kufafanua dosari hizo, hatua tano muhimu huzingatiwa: (i) kukusanya sampuli ya lugha ya wajifunzaji, (ii) kubainisha dosari, (iii) kufafanua dosari, (iv) kutafuta kiini cha dosari na (v) kutathmini dosari. Katika makala hatua ya kwanza hadi ya nne ilizingatiwa. Kwa kuzingatia kiunzi hiki, dosari lazima zibainishwe na kisha kutolewa maelezo ya kutokea kwake. Aidha, Corder (1971; 1974) aliainisha dosari katika makundi makuu manne ambayo ni: dosari za uongezaji, dosari za uondoaji, dosari za uteuaji na dosari za upangiliaji.

Ufafanuzi wa Dhana Muhimu

Katika jaribio la kufafanua suala la dosari za wajifunzaji lugha, Corder (keshatajwa) alitumia istilahi mbili; dosari na makosa. *Dosari* ni matokeo ya ujifunzaji usiokamilifu wa kanuni za kiisimu zinazofanywa na mjifunzaji lugha na kwamba dosari hizi hazikibishwa na mjifunzaji lugha mwenyewe. *Makosa* kwa upande mwingine, ni matokeo ya utumizi mbaya wa lugha kutokana na sababu mbalimbali kama vile uchovu, uzembe na kutojali kwa mjifunzaji kuhusu matumizi ya kanuni za lugha. Ufafanuzi huu unamaanisha kwamba, makosa yanatokana na mjifunzaji mwenyewe wakati dosari zinatokana na mbinu zilizotumika katika ufundishaji. Hii ina maana kuwa, dosari ziko nje ya uwezo wa mjifunzaji lugha ilhali makosa yako ndani ya uwezo wa mjifunzaji. Hii ina maanisha kwamba, mjifunzaji anakuwa anajua vyema kanuni na miundo ya lugha husika na anaweza kujirekebisha mwenyewe ikiwa uchovu, uzembe na kutojali hakutakuwapo. Makala haya yanaona kuwa dosari na makosa ni kitu kile kile, kwani dhana zote mbili yaani dosari na makosa zinahusu kukiuka kwa matumizi ya kanuni za Lg2 ambayo mjifunzaji anajifunza. Aidha, ni vigumu kupima ikiwa mjifunzaji Lg2 anajua kanuni na hapo anakosea kwa uchovu au uzembe kama Corder anavyodai.

Kuamili lugha na kujifunza lugha. Kuamili lugha ni mchakato unaofanyika katika hali ya ung'amuzibwete bila mhusika kukusudia. Krashen (1985) alihusisha mchakato huu na jinsi mtoto mdogo anavyopata Lg1. Kuhusu matokeo ya uamiliaji, muamiliaji lugha hupata umilisi wa lugha kwa kiwango karibu na wazawa. Richards na wenzake (1985) wanafasili dhana ya uamiliaji wa lugha ya pili kuwa ni mchakato ambao watu hujenga umilisi wa Lg2 au ya kigeni katika hali ya kutojitambua. Ellis (1986) anaeleza kuwa uamiliaji wa Lg2 ni mchakato changamani unaohusisha vitu vingi vinavyohusiana. Siti Khasinah (2014) anafasili uamiliaji wa Lg2 kuwa ni mchakato wa kujifunza Lg2 katika hali ya ung'amuzibwete ambapo mtu anapata Lg2 au lugha ya nyongeza (baada ya lugha ya kwanza).

Wakati ujifunzaji lugha ni mchakato wa makusudi unaofanywa na muhusika ili kujifunza lugha fulani; mchakato huu unahitaji jitihada na kujituma kwa muhusika ili kutimiza lengo lilikokusudiwa. Mchakato wa ujifunzaji lugha huchukua muda mrefu na wakati mwingine huweza kuchukua muda wote wa maisha ya mjifunzaji. Ni mchakato unaofanyika zaidi kwa watu wazima wanaojifunza Lg2.

Usasanyuzi dosari, ni njia ya kuainisha, kupambanua na kufafanua dosari zinazofanywa na mtu anayejifunza Lg2 au lugha ya kigeni. Aidha, Corder (1974) anafafanua dhana hii kuwa ni mchakato unojihusisha na ubainishaji wa kasoro za muamiliaji Lg1 na wajifunzaji wa Lg2 au ya kigeni. katika kushughulikia jambo hilo la dosari, wanausasanyuzi dosari hujishughulisha na mambo makuu manne: (a) jinsi mjifunzaji anavyoelewa lugha, (b) jinsi mjifunzaji anavyojifunza lugha, (c) matatizo anayokabiliana nayo mjifunzaji wakati anajifunza Lg2 au kigeni na (d) kung'amua mchakato wa ujifunzaji. Kwa ujumla mambo hayo yote manne hufanya kazi kwa pamoja.

Mitizamo ya watu wengine kuhusu Dosari za Wajifunzaji wa Lugha ya Pili

Tangu awali wakati taaluma ya usasanyuzi dosari inaanza, ilifungamanishwa na nadharia za ujifunzaji lugha zenye mweleke wa wanautabia. Ambapo, dosari za mjifunzaji zilichukuliwa kuwa ni matokeo ya kuwapo kwa mwingiliano wa kanuni na Lg1. Yaani dosari zilizofanywa na mjifunzaji Lg2 zilihusishwa na athari ya Lg1. Wanaisimu wenye mwelekeo wa kiusasanyuzi linganishi kama Lado (1957) walishikilia msimamo huo, kwamba dosari za Lg2 zinatokana na athari ya Lg1. Lado, kwa mfano, alikuwa analinganisha mifumo ya lugha mbili au zaidi kwa kuangalia zinavyofanana na kutofautiana, kisha kufanya ubashiri wa kitu ambacho kitatokea kwa mjifunzaji lugha husika. Matalani tuseme mzungumzaji wa lugha X anajifunza lugha Y ambayo kimundo ni tofauti na lugha yake X; kwamba atafanya dosari katika lugha Y kwa sababu ya uhawilishaji wa kanuni za lugha X na kuzitumia katika lugha Y, na hivyo kusababisha dosari za kimundo katika Lg2. Mtazamo huu ulishika mwishoni mwa miaka 1940 na mwanzoni mwa miaka ya 1960. Baadaye kidogo, ilibainika wazi kwamba mwelekeo huu wa usasanyuzi linganishi ulishindwa kutoa maelezo toshelevu baadhi ya dosari mbalimbali za mjifunzaji Lg2. Ilibainika wazi na watafiti mbalimbali kama vile Corder (1967; 1974), Gass na Selinker (2008), Wei (2010) na Gawasike (2016) kwamba, dosari za mjifunzaji lugha hazitokani hazitokana tu na mwingiliano baina ya Lg1 na Lg2 ila masuala mbalimbali ya kimajumui kuhusiana na miundo ya lugha yaliyoelekea kusababisha dosari kwa wajifunzaji lugha. Utambuzi alionao mjifunzaji na mambo mengine kuhusu muundo wa lugha ndiyo husababisha dosari kwa mjifunzaji lugha. Kulingana na Kashavarz (2003, 2006), usasanyuzi dosari umegawanyika katika matawi makuu mawili yaani Kiunzi cha Usasanyuzi Dosari na Usasanyuzi Tumizi wa Dosari.

Kiunzi cha Usasanyuzi Dosari

Hiki ni kiunzi kinachojaribu kutafuta na kupambanua matatizo mbalimbali yanayohusiana na ujifunzaji Lg2 na utokeaji wa dosari husika. Yaani kiunzi kinaangalia uhusiano wa mazingira ya kujifunzia Lg2, mtazamo wa mjifunzaji na mikakati ya ufundishaji inavyoelekea kuchangia dosari. Pia, kiunzi hiki kinatalii miundo na mifumo inayofanya kazi katika mchakato wa kujifunza Lg2. Kadhalika, kiunzi hiki kinachunguza sababu ya dosari katika mchakato wa ujifunzaji. Aidha, kinajihusisha na kubainisha aina ya wajifunzaji wa Lg2 ambao wanategemewa kufanya dosari ikilinganishwa na wajifunzaji wengine. Kwa kuzingatia aina ya wajifunzaji, ilihitimishwa kwamba watu wazima wanaojifunza Lg2 wana uwezekano mkubwa wa kufanya dosari nyingi kuliko watoto wadogo kwa sababu ya mwingiliano wa kanuni kati ya Lg1 dhidi ya ile wajifunzayo. Hivyo, kuhusiana na dosari kiunzi hiki kinachunguza dosari kwa mawanda mapana zaidi na siyo tu kuhusisha na Lg1 kama ilivyokuwa ikifanywa na wanausasanyuzi linganishi.

Usasanyuzi Tumizi wa Dosari

Tawi hili la usasanyuzi dosari linajikita zaidi katika kutafuta suluhisha la dosari zinazotokana na ufundishaji wa Lg2. Kwa maana ya wazi ni kuwa, wana usasanyuzi dosari tumizi wanatambua kuwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lg2 hutokea dosari mbalimbali. Dosari hizi zinaweza kuwa kwa upande wa mfundishaji au mjifunzaji. Hivyo, tawi hili linashughulikia jinsi ya kukabiliana na dosari hizo. Aidha, tawi la usasanyuzi tumizi dosari ni tawi linalojihusisha na utengenezaji wa zana za kujifunzia Lg2 pamoja ubunaji wa kozi au masomo ya muda wa ziada, ili kuwasaidia wajifunzaji Lg2. Bailey (1985) na Krashen na Tarrell (1985) ni miongoni mwa wafuasi wa tawili hili. Kwa kifupi hili ni tawi la usasanyuzi linganishi linalojihusisha na mbinu mbalimbali atumiazo mwalimu kufundisha Lg2 na jinsi ya kukabiliana na matatizo yenye kuambatana kwayo. Makala haya yanashughulikia dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na sekondari nchini Tanzania, jamii ya Wakinga ikitumiwa kama mfano. Makala yanabainisha aina mbalimbali za dosari zinazofanywa na wanafunzi hawa na kujielekeza katika kuchunguza sababu za dosari hizo. Hivyo, kiunzi cha usasanyuzi dosari ndicho kimezingatiwa na makala haya.

Uhistoria wa Maendeleo ya Taaluma ya Usasanyuzi Dosari

Kama ilivyodokezwa hapo juu, katika kipindi cha miaka ya 1940 usasanyuzi dosari ulichagizwa na ujifunzaji lugha ulioegemea katika nadharia za wanautabia; ambapo dosaria zinazofanywa na mjifunzaji Lg2 zilihusishwa na atharia za kanuni za Lg1. Ilichukuliwa kuwa ujifunzaji Lg2 ni mchakato wa ujenzi na kuimarika wa tabia, na kwamba tabia (kanuni) za lugha moja ikishaanza inasababisha ukinzania katika kujifunza tabia (kanuni) za Lg2 au ngeni.

Usasanyuzi linganishi ulifanyika kwa kutazama dosari za mjifunzaji lugha kwa kutalii kanuni za lugha zote mbili. Ikiwa kulikuwa na ufanano baina ya kanuni au miundo ya lugha hizi mbili basi uhawilishaji chanya hutokea. Yaani ukinzani hautatokeana ikiwa kuna mwachano baina ya kanuni au miundo ya lugha hizi mbili, uhawilishaji hasi hutokea kwa mjifunzaji; yaani ukinzania hutokea. Kwa ujumla, katika kipindi cha miaka ya 1940 dosari za wajifunzaji wa Lg2 zilinasibishwa na athari za Lg1 (Ellis, 1995; Norrish, 1983; Şanal, 2007; Gass na Selinker, 2008; Kazemian na Hashemi, 2014).

Ifahamike kwamba Nadharia ya Usasanyuzi Linganishi haikuweza kueleza sababu zote za dosari za mjifunzaji Lg2. Aidha, tafiti za baadaye zilizoongozwa na Chomsky katika Nadharia yake ya Uhulka, zilibaini kuwa mchakato wa dosari si rahisi kueleza kama wanausasanyuzi linganishi wanavyouchukulia. Nadharia ya Uhulka ilikuja na mtazamo kwamba, katika kujifunza Lg2 kuna michakato ya utambuzi mbalimbali ambayo huandamana na ujifunzaji lugha; kama vile motisha, mtazamo na athari za kijamii. Hivyo, michakato tambuzi ina nafasi muhimu kabisa katika kuamua ikiwa mjifunzaji wa Lg2 atamudu lugha husika au la. Mchakato wa kujifunza Lg2 ni suala changamani na kwamba usasanyuzi dosari ni usasanyuzi isimu. Kwa maana kwamba michakato ya dosari za mjifunzaji Lg2 ni changamani mno, kwani kuna baadhi ya mambo ambayo yapo nje ya lugha ya mjifunzaji kama motisha na mtazamo.

Dosari zinazofungamana na wajifunzaji wa Lg2

Zipo sababu mbalimbali za dosari miongoni mwa mjifunzaji Lg2. Sababu mojawapo ya dosari za wajifunzaji Lg2 yaweza kuwa uhaba wa vifaa vya kujifunza lugha au upungufu wa vifaa vya kufundishia kwa mwalimu. Miongoni mwa sababu nyingine zilizobainishwa na watafiti kama vile James (1989, 1998) Ellis (1995) Ziahosseiny (1999) Kashavarz (2003, 2006) Şanal (2007) Darus (2009) Kazemian & Hashemi (2014) kuhusu chanzo cha dosari kwa wajifunzaji lugha ni:

Uhawilishaji lugha, ujumuivuwa kanuni, urahisishajiwa kanuni, utumizi kidogo, ukakamaaji, Kutokuwa na maarifa ya lugha na mwingiliano na lugha nyingine.

Uhawilishaji lugha

Ni sababu inayotokea zaidi katika mazingira ya ujifunzaji wa lugha moja tuseme Lg2 ambapo mjifunzaji lugha huyu tayari anayo lugha nyingine tuseme Lg1. Katika mazingira hayo mjifunzaji Lg2 huyu huelekea kuhamisha kanuni za Lg1 na kuzitumia katika Lg2. Kwa lugha nyepesi, uhawilishaji ni hali ya mjifunzaji wa Lg2 kuhamisha kanuni na miundo ya Lg1 na kuitumia katika mfumo wa Lg2. Uhawilishaji lugha hutokea kwa namna mbili, chanya na hasi. Ikiwa lugha mbili zinazohusika zinafanana kimuundo na kimfumo uhawilishaji chanya unaweza kutokea. Yaani mjifunzaji wa Lg2 atakapohamisha kanuni za Lg1 na kuzitumia

kujifunza lugha anayojifunza hakuna dosari zitakazotokea kutokana na kufanana kwa lugha hizo. Wakati, uhawilishaji hasi hutokea pale ambapo kimuundo na kimfumo Lg1 si sawa na Lg2. Yaani mjifunzaji wa Lg2 atakapohawilisha kanuni za Lg1 na kuzitumia katika Lg2 atasababisha dosari. Kulingana na Selinker (1972) uhawilishaji lugha ni utumizi wa kanuni za lugha moja katika kujifunza lugha nyingine.

Ujumuiwu wa Kanuni

Hii ni hali ambayo mjifunzaji wa Lg2 huhamisha kanuni moja na kutumia katika mazingira yote ya lugha ambapo kanuni hiyo hufanya kazi katika mazingira fulani tu. Ni upanujaji wa matumizi ya kanuni moja katika mazingira ambapo kanuni hiyo haikubaliki. Hii huwa ni chanzo cha dosari kwa wajifunzaji wa Lg2 au ya kigeni. Kwa mfano, uzoefu wa kufundisha Kiswahili ikiwa ni lugha ya kigeni kwa wanafunzi wageni ambao Lg1 ni Kiingereza unaonesha kuwa wajifunzaji hawa hufanya dosari zifuatazo:

A. Lg1 (Kiingereza)

1. I am in Dar es Salaam
2. I am going to Arusha
3. I am not eating

B. Lg2 (Kiswahili)

- * Nipo katika Dar es Salaam
- * Ninakwenda cha/kwa Arusha
- * Sikuli

Chanzo: Utafiti (2017)

Dosari zilizobainishwa katika safu B ni mfano wa dosari za ujumuiwu wa kanuni za Lg1 katika Lg2. Mwanafunzi ametumia utaratibu wa Lg1 katika Lg2 na kusababisha dosari. Akishadidia hili, James (1998) anaeleza kwamba hali hii pia hutokea kwa watoto wadogo wanapojifunza Lg1. Ni katika welekeo huo, ndiyo maana wana usasanyuzi linganishi walihitimisha kwamba dosari za wajifunzaji wa Lg2 zinasababishwa na athari za Lg1.

Urahisishaji wa Kanuni

Hii inahusu mjifunzaji wa Lg2 kukwepa kutumia kanuni changamani na kupendelea kutumia kanuni za kawaida na nyepesi. Sababu huu hii pia hujulikana kama dosari kutokana na sababu ya uepukaji. Hali hii ya mjifunzaji kukwepa kutumia kanuni na miundo changamani husababisha kutokea kwa dosari. Kwa mfano, katika jamii ya Kihaya kuna changamoto ya kutamka silabi *ng'a* na *ha*. Hivyo, wajifunzaji na watumiaji wa lugha ya Kiswahili katika jamiilugha ya Wahaya, huelekea kukwepa kutamka silabi hizo wanapozungumza lugha ya Kiswahili, hata katika mazingira ambamo ni lazima kuzitumia silabihizo. Aidha, katika utafiti uliofanyika mwaka 2016 kuhusu wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili ikiwa ni Lg2 katika jamii ya Wakinga, walionekana kukwepa kutumia urejeshi unaojitokeza mwishoni mwa kitenzi na urejeshi unaotumia *amba*. Watoa taarifa wote walitumia namna moja tu ya kudhihirisha urejeshi katika Kiswahili. Aidha, data zilionesha watoa taarifa walikwepa kutumia mofu ya hali //hu// ambyo

kimsingi ilikuwa ni mofu ya lazima katika kueleza matukio ya hali ya mazoea. Kukwepa au kurahisisha huko kulisababisha dosari mbalimbali (taz. Gawasike, 2016).

Ukakamaaji

Dhana ya ukakamaaji imeelezwa na watalaamu mbalimbali miongoni mwao akiwa ni Han (2013) ambaye anasema kwamba inahusu dosari sugu anazozipata mjifunzaji wa lugha. Dosari hizo haziwezi kubadilika licha kurekebishwa. Ni hali ya mjifunzaji wa Lg2 au ya kigeni kushindwa kuvuka katika hatua ya lugha darajia. Lugha darajia ni lugha ya mpito ambayo mjifunzaji wa Lg2 hujitengenezea kabla ya kumudu kanuni za lugha anayojifunza. Kwa kawaida *lugha darajia/lugha mpito*² huwa ni ya muda maalumu na yenye dosari mbalimbali. Wajifunzaji wanaposhindwa kubadili dosari hizo zilizokuwa zinafanywa kipindi cha mpito licha ya maelekezo mbalimbali wayapatayo kutoka kwa walimu au licha ya kufundishwa na kuwa na fursa mbalimbali za kufanyia mazoezi. Hali hiyo ya kutovuka katika hatua ya lugha mpito hujulikana kuwa ni kukakamaa. Dosari hizi zinaweza kujidhirisha katika viwango mbalimbali vya lugha, kuanzia kiwango cha sauti hadi kilongo (Wei, 2008). Katika utafiti uliofanyika miongoni mwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wakinga, dosari za ukakamaaji zinajitokeza zaidi katika kiwango cha fonolojia, mofolojia na sintaksia.

Kutokuwa na maarifa ya lugha husika

Hii ni dosari ambayo inatokea kwa sababu mjifunzaji wa lugha hajui kanuni na wala hana maarifa ya lugha kuhusu kipengele anachokutumia katika kufanya mawasiliano. Hali hii husababisha mjifunzaji kufanya dosari anapozungumza au kuandika kwa kutumia Lg2. Hali hii humtatiza mjifunzaji lugha. Ni miongoni mwa sababu za dosari kwa wajifunzaji wa Lg2. Wakati mwingine wajifunzaji lugha hufanya dosari kutokana na kukosa au kutojua kanuni za lugha inayohusika. Makala haya yanaangazia dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wakinga kwa kuzingatia sababu na mitazamo wa usasanyuzi dosari. Makala haya yanajaribu kuangazia nafasi ya usasanyuzi dosari katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lg2.

² Ni aiana ya lugha ambayo mjifunzaji wa lugha ya pili au ya kigeni hujiundia kabla ya kufikia umilisi wa lugha anayojifunza/amili. Kwa kawaida lugha darajia au lugha mpitio huambatana na dosari mbalimbali za kimuundo, kimaana na kimofolojia.

Dosari za Uongezaji

Ni dosari inayorejelea uongezaji wa kipengele chochote cha kisarufi kama vile: mofu, sauti au silabi katika mazingira ambayo kipengele hicho hakitakiwi kuwapo. Katika utafiti uliofanyika katika jamii ya Wakinga wanaojifunza Kiswahili ikiwa ni Lg2 hali hii pia ilijitokeza ambapo wajifunzaji waliongeza sauti /-u-/ na sauti /n-/ kama nukuu ifuatayo inavyoonesha. Neno lililokozwa wino linathibitisha hali hiyo.

“NinapoamUka asubuhi kwa sababu mimi ni mwanafunzi ninamUka saa 10:00 kusoma...TunapumUNzika saa nne, tunaingia darasani kusoma. TunapumUNzika saa sita,”

Chanzo: Uwandani (2017)

Dosari za Uondoaji

Ni dhana inayorejelea kuondoa au kutoa kipashio fulani cha kisarufi katika mazingira ambamokipashio hicho ni muhimu na kinahitajika ili kukamilisha muundo wa lugha. Data zilizokusanywa kwa njia ya insha kutoka kwa wajifunzaji wa Lg2 katika jamii ya Wakinga zilionesha dosari hizo za uondoaji. Jedwali na 1.1 na nukuu vinathibitisha hali hiyo.

“...alafu nikitoka kusoma saa 12 ninafanya usafi wa nje na ndani alafu nikishafanya usafi huo naoga, navaa nguo za shule alafu natandika kitanda, nachukua mfuko wa shule naanza kwenda shuleni.

Chanzo: Uwandani (2017)

Jedwali Na. 1.1: Udondoshaji wa Fonimu /h/

Neno la Kiswahili sanifu	Muundo
Halafu	Øalafu
Lugha	lugØa
Gharama	gØarama
Ghafla	gØafla

Chanzo: (Uwandani, 2017)

Kama jedwali linavyoonesha pamoja na nukuu, wajifunzaji wa Lg2 hudondosha mofu //-(h)-// inapotokea sehemu yoyote katika neno. Ikiwa mwanzo au katika mwa neno hudondoshwa. Hali hii husababisha dosari miongoni mwa wajifunzaji wa Lg2 kwa kuzingatia kanuni za Kiswahili.

Dosari za Uteuaji

Hizi ni zile zinazotokana na uteuzi usiosahihi wa miundo fulani ya lugha. Wajifunzaji wa lugha ya Kikinga walidhihirisha dosari hizi ambapo kulikuwa na uteuzi mbaya wa viunganishi kama nukuu ifuatayo inavyoonesha:

“Namka asubuhi na mapema saa 11 kamili naenda kusoma alafu, ...alafu nikishafanya usafi huo naoga, navaa nguo za shule alafu, ...”

Chanzo: Uwandani (2017).

Aidha, licha ya kuwa nukuu ya viunganishi vilivyoteuliwa kutumika katika insha husika vimekosewa kwa kuandikwa kwa kuondosha mofu //h-// pia, mahala vilipowekwa katika sentensi sio sahihi.

Dosari za Upangiliaji (muundo)

Ni dosari zinazotokana na mpangilio mbaya wa maneno katika sentensi au tungo. Wajifunzaji Kiswahili katika jamii ya Wakinga hufanya dosari za upangiliaji wa maneno. Hutoa tungo ambazo hazina upatanisho wa kisarufi. Katika uchunguzi uliofanyika kwenye insha za wajifunzaji wa Lg2 katika jamii ya Wakinga, ilibainika hali ya utungaji wa sentensi zisizo na upatanisho wa kisarufi kama mifano ifuatayo inavyoonesha:

- i. "...nasikiliza walimu atasema nini"
- ii. "...mimi ni wanafunzi wa kidato cha pili"
- iii. "...naelekea mstarini, tunafanya usafi"
- iv. "...mwalimu anaturuhusu kuwa niende nyumbani"

Chanzo: (Uwandani, 2017)

Tungo hizo zimedondolewa kutoka kwenye insha zilizoandikwa na wajifunzaji wa Lg2 kuanzia darasa la tano hadi kidato cha nne. Aidha, kimuundo, tungo hizi hazikubaliki kwa mujibu wa kanuni za lugha ya Kiswahili sanifu. Dosari hizi zilifanywa na wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili kutokana na upangiliaji mbaya wa vipashio.

Ujifunzaji lugha wa Lg2 katika Jamii ya Wakinga

Mingoni mwa malengo mahususi ya utafiti ilikuwa ni kufafanua sababu za dosari sugu zinazotokea kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wakinga. Katika kuhakikisha lengo hili linafikiwa, watoa taarifa wanafunzi wa shule za msingi kuanzia darasa la tano hadi la saba na wanafunzi wa shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne walijaza hojaji. Hojaji ililenga kupata maoni yao kuhusu changamoto wanazozipata katika kujifunza lugha ya Kiswahili wakiwa katika mazingira waliyopo. Aidha, walimu wa shule za msingi na sekondari wanaofundisha Kiswahili walishiriki katika mahojiano. Uchunguzi uliofanywa na utafiti huu ulibainisha sababu zifuatazo kuwa ndizo zinazosababisha hali ya dosari kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Jedwali lifutalo linaonesha kwa muhtasari chanzo cha dosari kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili:

Jedwali Na.1. 2: Sababu za Dosari kwa Wajifunzaji wa Lg2

Sababu za Dosari kwa Wajifunzaji wa Lg2		Kiwango cha dosari kwa Asilimia		
		Zaidi ya 20%	Kati ya 10-19%	Pungufu ya 10%
1.	Athari za Lugha mama/Kikinga	√√√		
2.	Muda mwingi huongea Kikinga	√√√		
3.	Ukosefu wa mwingiliano baina ya Wakinga na jamii nyingine		√√	
4.	Tofauti ya Kikinga na Kiswahili		√√	
5.	Kuchelewa kuanza kujifunza Kiswahili miongoni mwa Wakinga			√
6.	Mazingira hayawezeshi ujifunzaji wa Kiswahili		√√	
7.	Tofauti ya kimsamiati kati ya Kikinga na Kiswahili	√√√		
8.	Ukosefu wa vyombo vya habari			√

Chanzo: (Uwandani, 2017)

Ufunguo: Alama hii √√√ inaonesha kuwa sababu hizi zilijitokeza kwa zaidi ya asilimia 20, katika kusababisha dosari; alama √√ ni kuwa sababu hizi zimejitokeza kati ya asilimi 10-19 na alama √ ni kwamba sababu husika zimejitokeza kati ya asilimi 0-10 . Kama jedwali linavyoonesha kuna sababu mbalimbali zinazosababisha hali ya dosari kwa wajifunzaji wa Lg2 katika jamii ya Wakinga. Kwa mfano athari za Lugha mama/Kikinga na muda mwingi kutumia lugha ya Kikinga zilidhihirika kuchangia zaidi hali ya dosari kwa wajifunzaji wa Lg2 kuliko kuchelewa kuanza kujifunza lugha ya Kiswahili na ukosefu wa vyombo vya habari. Vilevile, katika kudhihirisha kwamba wajifunzaji wa Lg2 katika jamii ya Wakinga hufanya dosari mbalimbali, uchunguzi uliofanywa na utafiti huu unaonesha kuwa chanzo kikubwa cha dosari hizi ni tofauti kati ya Lg1 na Lg2 pamoja na wajifunzaji wa Lg2 kushindwa kumudu vipengele vya Lg2.

Upangiliaji wa Data

Kwa kuzingatia dosari zilizojitokeza kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wakinga, dosari za wajifunzaji ziko katika aina kama zilivyoainishwa na Corder (1974), dosari za uongezaji, dosari za uondoaji, dosari za uteuaji na dosari za upangiliaji. Imebainika pasi shaka kwamba, wajifunzaji

wa Lg2 katika jamii ya Wakinga hufanya dosari mbalimbali za kisarufi kutoka na ama kutojua kanuni za sarufi ya Kiswahili au kutokana na athari za Lg1. Usasanyuzi linganishi uliofanywa hasa kupitia insha za wajifunzaji lugha unaonesha dosari zilizofanywa na wajifunzaji lugha hawa zinadhihirisha ufafano na utofauti baina ya lugha hizi mbili yaani Kikinga na Kiswahili. Aidha, usasanyuzi linganishi unadhihirisha umbali wa kiisimu baina ya lugha hizi mbili. Dosari ya udondoshaji wa kiambishi nafsi katika kitenzi ndiyo dosari iliyobainika kupitia insha za watoa taarifa. Dosari za uchopekaji wa sauti /-u-/ na /-n-/ pia imejitokeza zaidi. Kadhalika, dosari za udondoshaji wa sauti /-h-/zimejitokeza. Vilevile dosari za ukosefu wa upatanisho wa kisarufi kati ya kiima na kiarifu katika tungo zimebainika kufanywa na wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wakinga. Jedwali lifuatalo linabainisha kwa muhtasari dosari hizi:

Jedwali Na. 1. 3: Aina za Dosari

Udondoshaji	Uteuaji	Uongezaji	Mpangilio
Øalafu	Lambi/lambi	ninamuka	i. ...nasikiliza walimu atasema nini
lugØa	mfua	Tunapumunzika	ii. ...naelekea mstarini, tunafanya usafi
gØarama	fisia gali/lifti		iii. ...mimi ni wanafunzi wa kidato cha pili
gØafla	amli ya kijiji		iv. ...mwalimu anaturuhusu kuwa niende nyumbani
	semanini/samanini/femanini		

Chanzo: (Uwandani, 2017)

Jedwali linavyoonesha kuwa wajifunzaji Kiswahili katika jamii ya Wakinga hufanya dosari mbalimbali ikiwamo za udondoshaji, uteuzi, uongezaji wa vipashio na mpangilio mbaya wa tungo. Nyingi ya dosari hizo ni za kifonolojia, za kimofolojia na pia za kimuundo. Hivyo, dosari hizi zinaakisi maelezo ya Wei (2008) kuwa dosari za wajifunzaji wa Lg2 hujitokeza katika viwango mbalimbali.

Hitimisho

Data za makala haya ni kutoka uwandani, wilaya ya Makete katika mkoa wa Njombe. Mbinu zilizotumika kukusanya data ni hojaji na uandishi wa insha. Makala haya yameeleza dhana ya dosari na kuonesha dosari mbalimbali zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika jamii ya Wakinga. Pia, yamefafanua mikabala miwili ambayo imekuwa ikitumika kufafanua chanzo cha dosari za wajifunzaji wa Lg2. Sababu za dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lg2 zimeoneshwa na kisha kukazia kuwa athari za Lg1 ndiyo

husababisha dosari mbalimbali hasa za dosari za udondoshaji wa kiambishi nafsi. Hata hivyo, makala yameonesha kuwa hiyo siyo sababu pekee ya kusababisha dosari kwa wajifunzaji wa Lg2. Kuna sababu zingine kama vile ukosefu wa maingiliano kati ya jamii ya Wakinga na wazungumzaji wa wazawa wa Kiswahili, ukosefu wa ingizo.

Marejeleo

- Bailey, K. M. (1985). "Classroom centered research on language teaching and learning". Katika M. Celce-Murcia (Mh.), *Beyond basics in TESOL: Issues and research in language teaching* (uk. 96-121). Rowley, MA: Newbury House.
- Corder, S. P. (1967). The significance of learners' errors. *Int. Rev. Appl. Linguist.*, 5, 161-169.
- Corder, S. P. (1971). *Idiosyncratic Dialects and Error Analysis* (uk. 14). Groos, Heidelberg. <http://dx.doi.org/10.1515/iral.1971.9.2.147>.
- Corder, S. P. (1974). *Error Analysis*. Katika J. P. B. Allen, na S. Pit Corder (Wah.), *Techniques in Applied Linguistics*. London: Oxford University Press.
- Darus, S. (2009). Error analysis of the written English essays of secondary school students in Malaysia: A case study. *Eur. J. Soc. Sci.*, 8(3), 483-495.
- Ellis, R. (1995). *Understanding Second Language Acquisition*. Oxford: OUP
- Gawasike, A. (2016). Ukakamaaji kwa Wajifunzaji wa Lugha ya Kiswahili katika Jamii ya Wakinga. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapwa): Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Gass, S. M., na Selinker, L. (2008). *Second Language Acquisition: An introductory course*. New York and London: Routledge.
- Han, Z. H. (2013). "Forty years later: Updating the Fossilization Hypothesis". *Katika Language Teaching*, 2 (46), 133-171.
- James, C. (1989). *Contrastive Analysis*. London: Longman.
- James, C. (1998). *Errors in Language Learning and Use*. London: Longman.
- Kazemian, B., na Hashemi, S. (2014). A contrastive linguistic analysis of inflectional bound morphemes of English, Azerbaijani and Persian languages: A comparative study. *Journal of Education & Human Development*, 3(1), 593-614.
- Keshavarz, M. H. (2003). *Contrastive Analysis and Error Analysis*. Tehran: Rahnama Publications.
- Keshavarz, M. H. (2006). *Error Analysis: A Practical Course for English Students and Teachers*. SAMT, Tehran.
- Krashen, S. (1985). *The input hypothesis*. Harlow, Essex, UK: Longman.
- Krashen, S. na Terrell, T. D. (1983). *Natural Approach Language Acquisition in Classrooms*. Great Britain: Prentice Hall International.
- Norrish, J. (1983). *Language Learners and Their Errors*. Macmillan Publishers.

- Richards, J. C. (1971). A noun-contrastive approach to error analysis. *English Language Teaching*, 25(3), 204-219. <http://dx.doi.org/10.1093/elt/XXV.3.204>
- Richards, J. (1974). *Error Analysis and Second Language Strategies*. Longman.
- Şanal, F. (2007). A Learner Based Study on Second Language Lexicology of Turkish Students of English. Tasnifu ya Uzamivu. Haijachapwa: Çukurova University.
- Skinner, B. F. (1957). *Verbal Behavior*. New York: Appletpn-Centuary-Crofts.
- Wei, X. (2008). "Implication of IL Fossilization in Second Language Acquisition". *KatikaEnglish Language Teaching*. Juzuu 1, China: Beijing Language and Culture University.
- Ziahosseiny, S. M. (1999). *A contrastive analysis of Persian and English and error analysis*. Tehran: Nashr-e Vira.